CHUO KIKUU CHA SOKOINE CHA KILIMO

# NDAKI YA MISITU WANYAMAPORI NA UTALII

## MTIKI - TEAK

(*Tectona grandis*)

Family: Verbenaceae












Kimetolewa na
Ndaki ya Misitu Wanyamapori na Utalii,
Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo,
S. L. P 3009,
Chuo Kikuu,
MOROGORO TANZANIA
Tel. Gen. Line 255 023 2603511/4
Ext. 4601
E-mail: forestry@suanet.ac.tz

## MAELEZO YA JUMLA

### UMRI WA KUKOMAA

Hutoa mbao zenye ubora ikifika umri wa miaka 30 - 50

### MATUMIZI :

Sakafu, fremu, vinyago, samani, mbao bora kwa kutengeneza boti n.k





### MATAYARISHO YA MICHE KWA AJILI YA KUPANDA

Weka mbegu katika gunia na uloweke katika maji (ni vizuri katika maji yanaayotiririka) kwa masaa 12. Kisha zitoe na uanike ukizitandaza katika jua kwa masaa 2 – 12. Rudia zoezi hili kwa siku 10 hadi 14 kabla ya kuotesha katika tuta kwenye kitalu (nursery).

Tuta liwe limenyanyuliwa cm.50 na litayarishwe kwa kutandaza cm. 5 za kokoto chini, cm. 35 za mchanga katikati kisha cm. 10 za mchanganyiko wa udongo na mbolea na kumalizia na mchanga uliotandazwa juu

Sukumiza mbegu kwenye tabaka la juu la tuta kisha nyeshea kwa maji mara mbili kwa siku. Mbegu huchipua baada ya siku 10 – 15 hadi siku 35 -45 na baadae hupungua. Mbegu ambazo hazijachipua huendelea kuchipua hadi mwaka unaofuata kama matunzo yataendelea vizuri. Kwa mwaka wa kwanza kuchipua ni 35%

## UPANDAJI

- Miche



- Visiki (stumps)



## UDONGO

- pH 6.5-7.5
- Unaoweza kuruhusu maji kupita na wenye madini ya calcium ya kutosha

## MATAYARISHO YA SEHEMU YA KUPANDA

- Shamba lifyekwe kuondoa magugu yote (miche ya Tiki huogopa magugu)



- Mistari ya kuotesha iwe imelimwa kufikia cm. 50 au mashimo yawe cm. 50
- Unyevu uwe wa kutosha kabla ya kuotesha miche

## NAFASI KATI YA MICHE

- Mita 3 kutoka mstari mmoja hadi mwingine na mita 3 mche baada ya mche (miche 1,680/ha)



- Kupunguzia (thinning) huwa inaweza kufanyika katika miaka ya 7, 11 na 15 hadi kufikia miaka 30 inapokuwa imekomaa vizuri kwa mbao.

